



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA**  
**WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA**  
**LESENI**



**TAARIFA KWA WAMILIKI WA KAMPUNI**

**“SULUHISHA NA BRELA”**

Dar es Salaam – 13 Juni, 2022

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imekuwa ikipokea malalamiko kutoka kwa Wanahisa na Wakurugenzi wa kampuni yanayohusu kutokuzingatiwa kwa matakwa ya Sheria ya Makampuni, Sura 212 pamoja na Katiba za uanzishaji wa kampuni wakati wa kufanya mabadiliko kwenye kampuni na pia malalamiko yanayotokana na uelewa mdogo wa matakwa ya Sheria ya Makampuni, Sura, 212.

BRELA inawataarifu Wakurugenzi na Wamiliki wa kampuni kwamba kuanzia tarehe 13 mpaka tarehe 19 Juni, 2022 itaendesha “Kliniki ya Biashara” kwa lengo la kusikiliza na kutatua changamoto za migogoro ndani ya kampuni, kujadiliana na kushauri kuhusu masuala yote yanayohusu uendeshaji wa kila siku wa kampuni wanazomiliki.

Zoezi hili litakuwa likianza saa tatu kamili asubuhi hadi saa kumi na moja jioni katika Ukumbi wa Mikutano uliopo Makumbusho ya Taifa, mtaa wa Shaaban Robert, mkabala na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) Dar es Salaam.

BRELA inawaomba Wakurugenzi na Wanahisa wa kampuni kutumia fursa hii kuleta changamoto zao ili kwa pamoja tuzijadili na kupata suluhisho la pamoja kwa lengo la kutengeneza mazingira mazuri ya ufanyaji biashara nchini.

**Imeandaliwa na:**

**KITENGO CHA HABARI NA MAWASILIANO**

